OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU
SHULE YA SEKONDARI MEATU

S.L.P 47
MWANHUZI – MEATU
Barua pepe: meatuhighschool2015@gmail.com
Mob. 0769-903890/0717-090789.

Kumb. Na: MSS/FS/JI/VOLI/2018 /01 Tarehe: ……..

Mzazi wa Mwanafunzi
……
S.L.P ……..……..…..
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MEATU WILAYA YA MEATU MKOA WA SIMIYU MWAKA 2018

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka wa masomo **2018/2019** tahasusi ya……. Shule ya Sekondari Meatu iko mkoa wa Simiyu wilaya ya Meatu. Umbali wa shule ni Km 5 magharibi kutoka Meatu mjini (Mwanhuzi) nje kidogo kutoka makao makuu ya Wilaya ya Meatu.Usafiri wa kuja shuleni unapatikana stendi ya mabasi Mwanhuzi ambao ni taxi na pikipiki, Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **02/07/2018** Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **30/06/2018 siku ya jumamosi** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/07/2018**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sare za shule

(a) Sare za shule hii ni suruali mbili za damu ya mzee (Esteem) kwa wavulana zenye marinda mawili upande wa mbele **(mtindo wa suruali modo hauruhusiwi)**
(b) Mashati mawili meupe ye tetroni mikono mirefu.
(c) Tai mbili ndefu za damu ya mzee(Esteem)
(d) T-shirt mbili za dark blue zenye kola nyeupe na T-shirt mbili za rangi ya kaki zenye kola ya dark blue
(e) Suruali mbili za rangi nyeusi kwa ajili ya kushindia (shamba dress)
(f) Viatu vya ngozi nyeusi visigino vifupi jozi mbili kwa wote. Viatu viwe vya kufunga na kamba na sio kuchomeka.
(g) Soksi nyeusi kwa wavulana
(h) Sare ya michezo kwa shule hii ni T-shirt ya orange na bukta ya blue kwa wavulana, viatu vya raba jozi moja
(i) Sweta mbili za uzi za rangi ya damu ya mzee(Esteem) zenye kola ya V
(j) Mkanda wa kuvalia suruali wa ngozi rangi nyeusi

NB; Mwanafunzi hatoruhusiwa kuja na nguo tofauti na sare ya shule na kuvaa nguo tofauti na sare ya shule awapo shuleni na mazingira mengine kipindi chote cha masomo yake hapa shuleni.

3.0 ADA NA MICHANGO YA SHULE

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000/=** na kwa muhula ni **35,000/=** fedha hizo zilipwe katika akauti ya shule **NA. 30901100045 NMB SHULE YA SEKONDARI MEATU** pamoja na michango ifuatayo:-

ADA	70,000/= (kwa mwaka)
TAALUMA	20,000/=(kwa mwaka)
WALINZI, WAPISHI NA VIBARUA WENGINE	30,000/=(kwa mwaka)
UKARABATI NA SAMANI	15,000/=
TAHADHARI	5,000/= (Non refundable fee)
MITIHANI YA KUJIPIMA(MOCK)	20,000/=
JUMLA NDOGO YA KULIPA BENKI	**160,000/=**

Jumla ya ada na michango ya kulipwa benki kwa muhula wa kwanza ni Tsh.125,000/= au 160,000/= kwa mwaka (Fedha hii lazima ilipwe benki ya NMB) pay in slip (stakabadhi ya benki ya NMB) iletwe kwa Mhasibu wa shule. Fedha hizo zilipwe
katika akauti ya shule NA. 30901100045 NMB SHULE YA SEKONDARI MEATU

4.0 MICHANGO INAYOLIPWA MOJA KWA MOJA KWA MHASIBU WA SHULE (DIRECT PAYABLE TO SCHOOL BURSAR)

KITAMBULISHO NA PICHA	6,000/=
HUDUMA YA KWANZA (5,000/=) NA BIMA YA AFYA(5,000/=)	10,000/=
NEMBO	2,000/=
JUMLA NDOGO YA KULIPA SHULENI	**18,000/=**
JUMLA KUU YA BENKI NA SHULENI	**178,000/=**

5.0 MAHITAJI MENGINE MUHIMU NA YA LAZIMA

Godoro futi 2 ½ na neti yenye dawa.
Shuka 2 za rangi ya Light bluu, blanketi 1, mto na taulo.
Sahani na bakuli za udongo na kijiko.
Counter books quire 4 kulingana na idadi ya masomo x 2 (masomo ya combination + 2 ya ziada yaani GS na jumla ni 8 counter books) na English Dictionary 1.
Dawa ya meno, sabuni za kufulia na kuogea.
Sanduku la chuma lenye kufuli ya kuaminika
Vitabu kulingana na masomo uliyochaguliwa kusoma na Faili 2 (spring files).
Bunda la karatasi (A4 Ream paper – 500 sheets)
Mifagio ya ndani yenye mpini na ya nje (soft and hard broom)
Ndoo 2 (lita 10)
Jembe jipya lenye mpini
Kwanja jipya
Panga jipya
Reki mpya yenye mpini, tochi inayotumia betri au mwanga wa jua kwa matumizi ya dharula
Dekio la kisasa (moper)
Mathematical set na scientific calculator.
Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia

TANIBIHI: Mwanafunzi hatapokelewa shuleni endapo hatakamilisha mahitaji muhimu ya shule yaliyoelekezwa kwenye fomu hii. Njoo na mahitaji yote na michango yote ili kuepuka usumbufu.Vilevile mwanafunzi aje na cheti cha kuzaliwa na result slip.

6.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya elimu sayansi teknolojia na mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni muhimu.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare za shule wakati unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
(i) Kutunza mali za umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

(a) Wizi
(b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
(c) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
(f) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
(g) Kufuga ndevu.
(h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(i) Uvutaji wa sigara
(j) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(k) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(l) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(m) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(n) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(o) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(p) Kudharau bendera ya Taifa.
(q) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(r) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

7.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

(a) Medical Examination Form itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni (Imeambatishwa pamoja na barua hii).
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule (imeambatishwa pamoja na barua hii).

"KARIBU SANA MEATU SEKONDARI"

Saini ya Mkuu wa Shule G. Bundala

Jina la Mkuu wa Shule GERVAS E. BUNDALA

Mhuri wa Mkuu wa Shule

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MEATU
S. L. P. 47
MWANHUZI – MEATU.

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU
SHULE YA SEKONDARI MEATU
S. L. P. 47
MWANHUZI - MEATU – SIMIYU.

TAREHE …….

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE NA AHADI ZA UTII
(Ijazwe kwa herufi kubwa na irudishwe kwa Mkuu wa Shule)

1. (a) Jina kamili: …….....
   (b) Tarehe ya kuzaliwa: …….....
   (c) Kijiji/Mtaa:…… Wilaya ……... ……
   Taifa: ……..
   (d) Dini: R. Catholic /Anglican/AICT/Lutheran/SDA/Moravian/Muslim n.k
   ……
   (e) Shule unayotoka: …….

2. Jina kamili la Baba/Mlezi: ……
   Anwani yake: ……
   Kazi ya Baba/Mlezi:……

3. AHADI ZA MWANAFUNZI

(a) Mimi ……
Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule. Nayakubali na niko tayari kuwa Mwanafunzi wa shule ya sekondari Meatu Sekondari.
Naahidi kwamba:
(i) Nitatimiza masharti yote ya shule
(ii) Nitatii sheria zote za shule. Nikikiuka ahadi zangu nitachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

TAREHE: ……. **…….....**
SAHIHI YA MWANAFUNZI

AHADI ZA MZAZI

Mimi …… (Mzazi/Mlezi) wa Mwanafunzi ……Nimeelewa maelekezo yote ya shule kwa mwanafunzi huyu.

Hivyo naahidi kwamba;
(i) Nitashirikiana kikamilifu na uongozi mzima wa shule katika kumuelimisha na kumlea ipasavyo.
(ii) Nitatimiza mahitaji yake yote ya shule.
(iii) Sitamkatiza masomo kwa minajiri ya shughuli za kifamilia, kumuoza, kumuozesha au mambo kama hayo yawezayo kumfanya aache shule.
(iv) Nitafanya kila jitihada kumwezesha mwanangu kuwahi shule kila siku na kufika shule siku ya kufungua shule bila kuchelewa.

TAREHE: …… **…….**
SAHIHI YA MZAZI

STUDENT'S MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster of Meatu High School)

Name of a Student: ……

Please examine the student named above and recommend if her/his health by responding to the following items. Kindly put a tick (✓) in front of each item, either YES or NO.

Does the student have problems in connection with: -

1. Sight? …… 1. No
   2. Yes
   If Yes, state ……

2. Hearing? …… 1. No
   2. Yes
   If Yes, state ……

3. Speech? …… 1. No
   2. Yes
   If Yes, state ……

4. T.B? …… 1. No
   2. Yes
   If Yes, state ……

5. Blood pressure? …… 1. No
   2. Yes
   If Yes, state ……

6. Any physical disability? …… 1. No
   2. Yes
   If Yes, state ……

7. Any other, state ? …… 1. No
   2. Yes
   If Yes, state ……

8. Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this school? …… 1. No
   2. Yes
   If No, state ……
   ……

……. **……**

Name and Signature **Designation**

Date: ……

MFANO WA SARE ZA WANAFUNZI

SARE ZA DARASANI

SHAMBA DRESS

SHAMBA DRESS